# LEARNING BY EAR 2012

## “Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 7: “Geuko la maadili"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WANAMTEMBELEA DKT. MAHIRO**

- **Malemba (MKE, 35)**
- **Mahiro ( MUME, 50)´**
- **MSIMULIZI**

**SCENE TWO: VALERIE AMRUDIA IRENE CHUONI**

- **Valerie (MKE, 19)**
- **Irene (MKE, 19)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE THREE: KAPAKA AMZURU DKT. MAHIRO**

- **Kapaka (MUME, 25)**
- **Mahiro (MUME,50)**

**SCENE FOUR: IRENE NA VALERIE KWA DKT. MAHIRO**

- **Mahiro (MUME, 50)**
- **Irene (MKE, 19)**
- **Valerie (MKE, 19)**

**UTANGULIZI:**

Hujambo na karibu tena katika Noa bongo, jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha nane katika hadithi ya **“Bado ningali mwanadamu”** – makala ya mchezo wa redio yanayoangazia matatizo ya wenye maradhi ya akili barani Afrika. Kukukumbusha iwapo ulipitwa na kipindi kilichopita: Malemba alimpeleka kijana wake Chumba kwa Dkt. Mahiro, mtaalamu wa maradhi ya akili pekee nchini, Mahiro alimshuku Chumba kuwa na maradhi ya urundifu wa akili unaojulikana kwa lugha ya kimombo kama ‘autism”. Na Irene alishangazwa na rafikiye Valerie alipomfuata chumbani kwake chuoni, baada ya kumkimbiza asimpate usiku kucha. Mwisho, Kapaka aliamua kutafuta msaada kutoka kwa Dkt. Mahiro alipogundua hatari iliyoko mbele yake: anaugua maradhi ya kurindimwa au Kiingereza hujulikana kama “depression”. Hebu tutabaruku yalioko katika kipindi hiki kwa jina **“Geuko la maadili**”.

Watufunguliao jamvi ni Valerie na Irene wakipata kifungua kinywa.

**SCENE ONE: VALERIE NA IRENE WAKIPATA KIFUNGUA KINYWA PAMOJA**

1. **ATMO:** **IN IRENE'S ROOM**

2. **SFX:** **TEA BEING POURED INTO A CUP**

3. **VALERIE:** Asante. Nashukuru, Irene. Ni nani angelinipa nguo zake. Sikujua kuwa chuoni vitu vyangu vyote vilichukuliwa na kuhifadhiwa stoo.

4. **IRENE:** Uhaba wa vyumba, ilibidi chumba chako kipatiwe mwanafunzi mwengine. Unajua sijawahi kuieleza halmashauri kuhusu hii hali yako. Isipokuwa wanafunzi wachache, wengi hawajui unachopitia.

5. **VALERIE:** Lakini nimerudi sasa. Nataka kuendelea na masomo yangu. Najihisi vyema.

6. **IRENE:** Valerie, sidhani kama hivyo ni sawa. Ulikuja hapa asubuhi ukiwa katika hali mbaya. Nafurahi na afueni yako sasa, lakini kwa muda gani, Val? Lisaa limoja au nusu siku? halafu urudiwe tena na hali hiyo. Vyema tumuone Dkt.

Mahiro. Tuko pamoja. Ukitaka nikusaidie tutasaidiana.

7. **VALERIE:** Bila shaka, niko tayari. Sitaki tena kuzisikia hizo sauti iwapo huyo daktari atanisaidia, basi sawa, twende. Niko tayari.

8. **IRENE:** Vyema. Nieleze, Valerie. Unapozisikia hizo sauti, huwa unaambiwa nini haswa? Na ni sauti za kike au za kiume?

9. **VALERIE:** Sifahamu. Huhisi woga. Pia huhisi walio karibu yangu wanaweza kudhurika.

10. **IRENE:** Ndiyo sababu ukanitoroka usiku ule?

11. **VALERIE:** Labda, sina hakika. Nimepitwa sana masomoni?

12. **IRENE:** Ndiyo, bila shaka Valerie, lakini usijali. Utarudi darasani iwapo daktari atakuruhusu. Uko tayari twende?

13. **VALERIE:** **(surprised)** Tayari? Tayari kufanya nini? Wanakuja tena….

14. **IRENE:** La hapana, yani ushanigeuka tena…Sasa nitaanzia wapi?

15. **MSIMULIZI:** Irene anapatwa na butwaa baada ya Valerie

kumjibu. Alifikiri rafiki yake ana nafuu! Endelea kusikiliza ujue kuliendeleaje. Katika mji huo huo, Malemba, anamweleza kakake Kalama kuwa kijana wake Chumba anaweza kuishi na hali hiyo maisha yake yote. Kalama, anayeamini dini sana, alifanya hima kuwaalika “wapendwa” kwa usiku wa mkesha ili kufukuza mapepo na majini kutoka kwa mpwa wake, Chumba.

**SCENE TWO: MKESHA WA MAOMBI NYUMBANI KWA KALAMA**

16. **(Kalama leads in singing a Christian song)**

17. **MALEMBA:** Kalama, Naomba tuongee nawe faragha? Tafadhali.

18. **KALAMA:** Ndugu – endeleeni kuimba na kuomba! Shetani leo tutamshinda usiku wa leo! Mtoto wa dadangu atakuwa huru kutokana na mapepo!

19. **SAUTI:** Amina! Amina! Amina!

20. **KALAMA:** Nipeni dakika chache.

21. **SFX: DOOR OPENING AND CLOSED**

22. **MALEMBA:** **(whisper)** Kalama nashukuru kwa haya unayofanya, lakini mbona hukunihusisha

kuhusu huu mkesha? Chumba hapendi halaiki! Hapendi wageni maishani mwake. Nimekueleza mara ngapi.

23. **KALAMA:** **(loud whisper)** Malemba, huyo si Chumba. Mapepo wanampinga asitangamane na sisi. Wanaogopa maombi na hawataki kumwachia. Lazima tumsaidie Chumba.

24. **MALEMBA:** Lakini Kalama, nilikwambia mtaalamu wa akili, Dkt. Mahiro, alinieleza hali hii ya Chumba haitibiki. Inaweza kudhibitiwa tu lakini haina tiba. Ana ugonjwa wa kurunda akili.

25. **KALAMA:** Kinachoshinda mwanadamu hakiwezi kushinda maombi. Amini na sisi dada, Chumba atawachwa huru na mapepo wanaomtatiza maishani mwake.

26. **MALEMBA:** Kalama, nilifikiri vivyo hivyo. Kabla ya daktari kunieleza kinaganaga, tungelifuata maagizo ya daktari. Tumfunze Chumba jinsi ya kuishi na hali hii, na nijifunze pia mimi jinsi ya kumhudumia yeye. Ijapo matibabu hayatamtibu lakini yatampa ahueni.

27. **KALAMA:** Sasa ulitaka mimi ni.….

28. **CHUMBA:** **(starts to shout and make strange noises in the next room)**

29. **MALEMBA:** Waona sasa! Hizo ni kelele za ukakamavu wake. Tafadhali waambie waache kuomba na kuimba.

30. **KALAMA:** Malemba, hayo ni mapepo, yanasikia joto la maombi. Tuwe kitu kimoja, hivi ni vita vikubwa! Lakini kwa ajili ya roho Mtakatifu tutashinda! Njoo, tujiunge na maombi.

31. **CHUMBA:** **(makes more strange and louder noises)**

32. **MSIMULIZI:** Waafrika wengi husadiki wazimu ni mkurupuko wa mapepo na majini. Dini nazo huchangia pakubwa kutatanisha watu. Alipogunduw ukweli uliopo, Malemba alitupilia mbali fikra zake na kuamulia matibabu. Lakini sasa kuna kakake Kalama, aliyekakamaa kuwa Chumba atapona pindi majini na mapepo watakapotoka. Kweli tutauona muujiza? Tulia tushuhudie. Kwa upande wa Kapaka, baada ya kukubali kumuona Dkt. Mahiro kwa ushauri na kuanza kumeza dawa dhidi ya sononi, anahisi ni muda muafaka sasa kurudia kufanya kazi yake ya zamani. Kwa hivyo, anaenda kumuona mkuu wake wa zamani,Bw. Patel.

**<u>SCENE THREE: KAPAKA RESUMES SEARCH FOR JOB</u>**

33. **ATMO:** **AT ALL-IN-ONE-SUPERMARKET (BUSY SUPERMARKET AMBIENCE)**

34. **KAPAKA:** Hujambo. Unajua hii ilikuwa sehemu yangu ya

kazi? Naitwa Kapaka, hata hivyo.

35. **MTOZA ADA:** Samahani, Nina kazi nyingi kwa sasa na sina muda wa maongezi.

36. **SFX: BEEPING SOUNDS AS WHEN GROCERIES ARE SCANNED**

37. **KAPAKA:** Hmmm...sawa…hamna tatizo. Lakini nitarudi. Hapo ni mahali pangu. Siendi popote mimi. Wewe endelea kunipashia kiti moto, sawa?

38. **MTOZA ADA:** Una wazimu, mwanamume! (to client), Subiri mnunuzi nipige simu.

39. **SFX: TELEPHONE BEING DIALLED**

40. **KAPAKA:** La, huna haja ya kupiga simu, namwendea Patel mimi mwenyewe ofisini kwake. Sina shaka hivi sasa ameshaniona kupitia kamera za ulinzi. Si nimekwambia, huyo mdosi anakuja.

41. **SFX: TELEPHONE RECEIVER BEING PLACED BACK**

42. **PATEL:** **(trying to act friendly)** Kapaka, mbona wewe nashangaza! Tafadali kuja ofisini kwangu.

43. **KAPAKA:** Habari, Bwana Patel? Nimerudi!

44. **PATEL:** Ninaona, hata nashangaa. Karibu…ingia ndani.

45. **SFX:** **DOOR CLOSED ABRUPTLY**

46. **PATEL:** **(changes tone)** Wewe unafikiria unafanya nini? Nilielezwa ulirukwa na akili, nilihisi mbaya, sikutarajia iwe hivyo. Sasa unatishia wafanyikazi wangu?

47. **KAPAKA:** La… hapana, Bwana Patel, hukunielewa. Kwanza kabisa, nilipoteza fikira zangu. Nikaumwa sana, kiasi cha kuamua… eh… unajua… kujitoa uhai.

48. **PATEL:** Om shanti shanti shanti!

49. **KAPAKA:** **(shocked)** Bwana Patel, tayari unatamani kama ningelikuwa nimekufa kwa lugha yenu?

50. **PATEL:** Hapana, maneno hayo kwa lugha yangu inamaanisha "amani kwa akili, maongezi na mwili". Unahitaji kuanza kujizoeza yoga. Inasaidia, hasa kwa akili. Itakusaidia.

51. **KAPAKA:** **(surprised)** Yoga? Unasema nini wewe? Nilikuja kukuomba unirudishe kazini kwangu.

Sio kuja kujifunza Kung-fu.

52. **PATEL:** **(offended)** Hei, Kung-fu iko na Wachina! Sikiliza, Kapaka, nasikitika hatuwezi kukuajiri. Kama iko na maradhi basi taambukiza wengine. Kama narejesha wewe kazini na hawa keshia wote na shika gonjwa, nani tahudumia kestoma? Nehi! Mimi pana weza saidia wewe.

53. **KAPAKA:** Patel, maradhi ya "depression" hayaambukizi...

54. **PATEL:** **(cuts him short)** *Bwana* Patel, kumbuka? BWANA Patel!

55. **KAPAKA:** Vyovyote vile, bwana! Nilifikiri ulisoma na unaelewa hivyo. Hiyo haiambukiziki.

56. **PATEL:** Rafiki yangu, hiyo ni sayansi inasema. Lakini iko ukweli ya mambo. Wale wanajua mambo ya mapepo wanajua.

57. **KAPAKA:** Bwana Patel, hii ni mara ya pili kunipuuza: Kwanza, ulinifuta kazi bila sababu, na sasa unanihujumu na maradhi yangu. Ninatumia dawa, na pia ninafanya mazoezi. Karibuni nitapoa, kama ninavyoamini. Na nitakapopona kamili, nitahakikisha kuwa nimekulipiza kisasi.

58. **PATEL:** Vitisho havitakusaidia lolote, Kapaka. Nenda kwa hospitali ya wendawazimu au ufanye yoga. Itasaidia hiyo. Kwa sasa pole, niko na kazi nyengine ya kufanya. Na usinisumbulie wafanyikazi. Ukithubutu nitakuitia askari polisi.

59. **KAPAKA:** Sijamalizana na wewe bwana PATEL, nitarudi!

60. **SFX:** **DOOR OPENED AND CLOSED**

61. **MSIMULIZI:** Moja ya kazi ngumu katika jamii ni kumrejesha mwenye kuugua maradhi haya ili akubalike na jamii. Wengi wa wauguwaji hawa hupoteza uaminifu kutoka kwa wandani wao. Kapaka ameanza kuona vile itamchukua muda mrefu kuweza kukubalika tena kazini. Anapoondoka ofisini kwa Patel kwenye lile duka alilokuwa akifanya kazi awali, Naye Irene na Valerie wako karibu na chumba cha utafiti cha Dkt.Mahiro.

## SCENE FOUR: IRENE NA VALERIE KWA DKT. MAHIRO

62. **ATMO:** **AT DR. MAHIRO’S EXAMINATION ROOM**

63. **MAHIRO:** **(calls out in a tired voice)** Mwengine ingia!

64. **SFX:** **CREAKING SOUND WHEN DOOR OPENS**

65. **MAHIRO:** Naam, niwasaidie nini wasichana?

66. **(IRENE AND VALERIE TALK AT SAME TIME)**

67. **MAHIRO:** Basi tuseme mmoja mmoja, tafadhali. Tumewahi kuonana kweli? Wewe mwembamba, namaanisha.

68. **VALERIE:** Tumekutana kweli? Sidhani … labda.

69. **IRENE:** Jina langu ni Irene, huyu ni rafiki yangu Valerie. Nyinyi wawili mmeshawahi kukutana. Alikuja hapa wakati alipoanza kusikia kelele. Sasa shida imezidi.

70. **MAHIRO:** **(remembering)** Ndio! Nilimwambia arudi, lakini hakurudi. Bila shaka lazima angelizidiwa. Niambie kumezidi nini, kwa sababu hata sasa hanonekani kama mtu wa akili kamilifu. Lakini anaonekana anatunzwa vizuri kwa ajili ya usafi wake.

71. **IRENE:** Nilijaaribu sana daktari, Valerie alinijia asubuhi akiwa nusu uchi.

72. **MAHIRO:** Mmmh…

**HITIMISHO:**

Na hapo ndipo kipindi chetu cha nane kinapotupa kisogo, katika hadithi hii ya wanaougua maradhi ya akili barani Afrika. Valerie anagundua sasa kuwa anaugua maradhi ya akili kwa jina la kitaalamu huitwa “skizofrenia”, ugonjwa mkuu wa akili ulio na ishara nyingi na mgumu kutibika. Je, Dkt. Mahiro atamsaidia kujinasua? Na huyu Kapaka kweli atapata ajira nyengine? Na hali ya Chumba itaboreka kweli? Kwa haya na mengineyo, utayapata katika kipindi kinachofuata. Ukitaka kusikiliza tena kipindi kilichotangulia tembelea tovuti yetu **dw.de/lbe**. Hadi wakati mwengine, Kwaheri kwa sasa.